



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA



TANGAZO KWA UMMA

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unakusudia kuuza miti katika Mashamba 11 ya miti ya kupanda katika mwaka wa fedha 2018/2019. Mashamba hayo ni Kiwira - Mbeya, Kawetire - Mbeya, Sao Hill - Mafinga, Ukaguru - Gairo, Shume - Lushoto, North Kilimanjaro - Tarakea, West Kilimanjaro - Hai, Meru/Usa - Arusha, Buhindi - Sengerema, Rubya - Ukerewe na Rubare - Bukoba. Maombi ya kuuziwa miti kwa wanaohitaji yatafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002, Kanuni zake za Mwaka 2004 Kifungu 31(i). Pia kwa kuzingatia tangazo la serikali namba 69 la Juni, 2006 kuhusu tasnia ya viwanda vya misitu nchini.

Hivyo, **wamiliki wapya** wa viwanda na misumeno ambao hawakuwepo wakati wa uhakiki wa mwaka 2016/2017 na wale ambao **walihakikiwa lakini kwa sasa wamebadili teknolojia** au wanakusudia kuhamisha biashara zao wanatakiwa kutuma fomu ya maombi ya kuuziwa miti kwa Meneja wa Shamba husika. Pia, wale wote **waliohakikiwa mwaka**

2016/2017 na kuuziwa malighafi na hatimaye kuvuna miti katika mashamba hayo katika msimu wa 2017/2018 na hawana mabadiliko kwenye biashara zao wanapaswa kujaza fomu ya maombi na kuituma katika shamba husika .

Mwisho wa kuwasilisha fomu ya maombi ni tarehe ya 25 Juni, 2018 saa tisa na nusu mchana. Fomu ya maombi inapatikana ofisi ya Meneja wa kila shamba na kwenye tovuti ya wakala. **Inasisitizwa** kuwa wale wote waliowekeza kwenye viwanda vya misitu na hawakujumuishwa kwenye orodha iliyohakikiwa na kutumika msimu uliopita kwa kila shamba wawasilishe vielelezo vyao kwa Meneja wa Shamba kwa ajili ya utambuzi **sambamba na maombi ya uvunaji.**

Imetolewa na:

MTENDAJI MKUU

WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

S L P 40832

Simu Na.: (255) (022) 2864249

Nukushi: (+255) (022) 2864257

DAR ES SALAAM

Tovuti: www.tfs.go.tz